JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

PROGRAMU YA KUENDELEZA SEKTA YA KILIMO AWAMU YA PILI (ASDP II)

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA KUENDELEZA SEKTA YA KILIMO AWAMU YA PILI (ASDP II) KWA MWAKA 2018/2019

DODOMA

JUNI, 2020

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Serikali inatekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II). Programu hii ni mwendelezo wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Kwanza ambayo ilitekelezwa mwaka 2006/2007 hadi mwaka 2013/2014. ASDP II ni Programu ya miaka kumi iliyoanza kutekelezwa kuanzia mwaka 2018/2019 na imepangwa kutekelezwa katika vipindi viwili vya miaka mitano hadi mwaka 2027/2028. Programu hiyo inatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali, Wadau wa Maendeleo na Sekta Binafsi. Kwa upande wa Serikali Programu hiyo inatekelezwa na Wizara za Sekta ya Kilimo (ASLMs) ambazo ni Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Wizara za Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Vilevile, watekelezaji wengine kwa upande wa Serikali ni Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Magereza na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa upande wa Jeshi la Kujenga Taifa.

Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili ina maeneo makuu manne ambayo ni: Usimamizi Endelevu wa Matumizi ya Maji na Ardhi kwenye kilimo, mifugo na uvuvi; Kuongeza Tija na Faida katika mazao, mifugo na uvuvi; Kuwezesha Upatikanaji wa Masoko na Uongezaji wa Thamani ya mazao katika Sekta ya Kilimo; na Kuiwezesha Sekta katika Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini. Maeneo haya manne yana jumla ya miradi ya kipaumbele kiutekelezaji 56. Gharama za utekelezaji wa Programu hii kwa mwaka wa kwanza (2018/2019) ilikadiriwa kuwa shilingi **2,268,351,449,399** ambapo Serikali na Washirika wa Maendeleo wana mgawanyo wa asilimia 41 sawa Shilingi **930,024,094,254** na Sekta Binafsi ilikuwa na asilimia 59 sawa na Shillingi **1,338,327,355,145.**

Utekelezaji wa Programu kwa kipindi cha mwaka 2018/2019, kwa upande wa Serikali na Washirika wa Maendeleo unaonesha kuwa jumla ya shilingi **445,587,907,297** ziliidhinishwa kwa ajili ya Programu ikiwa ni sawa na asilimia **48** ya fedha zilizotarajiwa kuidhinishwa kwa muktadha wa hitaji la bajeti ya program la Shilingi **930,024,094,254** kutoka Serikalini na kwa Washirika wa Maendeleo. Vilevile, kati ya fedha zilizoidhinishwa shilingi **243,854,258,959** zilitolewa, sawa na asilimia **55** ambapo kiasi cha shilingi **241,597,424,170** zilitumika ambazo ni sawa na asilimia **99** ya fedha zilizotolewa (Jedwali Na. 1). Hata hivyo, taarifa hii haioneshi mchango wa Washirika wa Maendeleo kwa miradi inayotekelezwa nje ya mfumo wa bajeti.

Kwa upande wa Sekta Binafsi kiasi cha shilingi 53,249,400,000 kiliwekezwa kwenye utekelezaji wa Programu kwa mwaka 2018/2019 hasa kwenye eneo la kukuza biashara na kuongeza thamani ya mazao. Kiasi hiki ni kidogo ukilinganisha na matarajio ya programu kwa uwekezaji unaopaswa kufanywa na Sekta Binafsi uliokadiriwa kuwa Shilingi **1,338,327,355,145**.

Jedwali Na. 1: MCHANGANUO WA FEDHA ZA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2018 - 2019

MAENEO MAKUU	Bajeti iliyoidhinishwa	Bajeti Iliyoidhinishwa (Tsh)		Bajeti iliyotolewa	Bajeti Iliyotolewa (Tsh)		Matumizi halisi	Matumizi Halisi Ya Bajeti (Tsh)	
		Fedha za Ndani	Fedha za Nje		Fedha za Ndani	Fedha za Nje		Fedha za Ndani	Fedha za Nje
ENEO LA KWANZA	56,626,094,000	30,441,116,000	26,184,978,000	13,783,630,000	4,751,380,000	9,032,250,000	11,830,236,495	4,751,380,000	7,078,856,495
ENEO LA PILI	74,926,179,280	58,806,663,280	16,119,516,000	34,002,069,121	30,659,711,323	3,342,357,798	33,728,627,837	30,659,711,323	3,068,916,514
ENEO LA TATU	251,458,767,531	225,530,780,000	25,927,987,531	193,624,028,665	173,484,680,000	20,139,348,665	193,624,028,665	173,484,680,000	20,139,348,665
ENEO LA NNE	62,576,866,486	62,076,866,486	500,000,000	2,444,531,173	2,444,531,173	-	2,414,531,173	2,414,531,173	-
JUMLA KUU	**445,587,907,297**	**376,855,425,766**	**68,732,481,531**	**243,854,258,959**	**211,340,302,496**	**32,513,956,463**	**241,597,424,170**	**211,310,302,496**	**30,287,121,674**

Aidha, taarifa imeainisha mafanikio na changamoto zilizopatikana katika utekelezaji na mapendekezo ya namna ya kutekeleza Programu kwa ufanisi zaidi kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Katika taarifa hii yameambatishwa majedwali yanayoonesha fedha zilizoidhinishwa, zilizotolewa na zilizotumika kwenye kazi zilizopangwa katika maeneo ya vipaumbele ya ASDP II. Vilevile, taarifa za fedha kwenye shughuli zilizopangwa zimeoneshwa kwa kina kwenye ***kiambatisho 1.***

SEHEMU YA PILI

2.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU KWA WIZARA ZA KISEKTA (ASLMs)

Katika mwaka 2018/2019, Wizara za Sekta ya Kilimo zimetekeleza Programu ya ASDPII kwa kuzingatia maeneo makuu manne kama ifuatavyo: -

2.1 Eneo Kuu la Kwanza: Usimamizi Endelevu wa Matumizi ya Maji na Ardhi

Lengo la eneo kuu la kwanza la ASDP II ni kuongeza usimamizi wa matumizi endelevu ya maji na ardhi kwa ajili ya mazao, mifugo na uvuvi. Vipaumbele vilivyozingatiwa katika eneo hili ni vinne ambavyo ni kuendeleza Mpango Maalum wa Matumizi ya Ardhi na Usimamizi wa Mwachano wa Maji; Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji; Kuendesha na Kusimamia Skimu za Umwagiliaji; na Kuwezesha Uendeshaji wa Vyanzo vya Maji kwa Ajili ya Mifugo na Samaki.

Katika kutekeleza Eneo Kuu la Kwanza la ASDP II, jumla ya Shilingi 56,626,094,000 ziliidhinishwa kwenye bajeti za Wizara za Sekta ya Kilimo kwa Mwaka wa fedha 2018/2019. Fedha zilizotolewa ni shilingi 13,783,630,000 sawa na asilimia 24 ya fedha zilizoidhinishwa. Jumla ya shilingi 11,830,236,495 zilitumika, sawa na asilimia 86 ya fedha zilizotolewa. (*Jedwali Na.2)*

Jedwali Na. 2: Vipaumbele na Bajeti katika Eneo Kuu la Kwanza (2018/2019)

	Vipaumbele na Bajeti katika Eneo Kuu 1: Usimamizi Endelevu wa Matumizi ya Maji na Ardhi			
	Eneo la Kipaumbele	**Fedha iliyoidhinishwa (TZS)**	**Fedha iliyotolewa (TZS)**	**Fedha iliyotumika (TZS)**
1	Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji	20,530,986,000	-	-
2	Mpango Maalum wa Matumizi ya Ardhi na Usimamizi wa Mwachano wa Maji	9,347,970,000	5,747,995,000	5,747,995,000
3	Kuendesha na Kusimamia Skimu za Umwagiliaji	19,820,458,000	5,065,635,000	3,112,241,495
4	Kuwezesha Uendeshaji wa Vyanzo vya Maji kwa Ajili ya Mifugo na Samaki	6,926,680,000	2,970,000,000	2,970,000,000
	Jumla ndogo	**56,626,094,000**	**13,783,630,000**	**11,830,236,495**

2.1.1 Kazi zilizotekelezwa

i. **Matumizi ya Ardhi na Usimamizi wa Mwachano wa Maji:**
Kuandaliwa kwa Hati za Haki Miliki za Kimila (CCRO) 141,687 katika Wilaya za Kilombero (74,896), Ulanga (33,035) na Malinyi (33,756) na Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji 120 katika Wilaya za Kilombero (49), Ulanga (38) na Malinyi (33). Pia kazi ya kupima mipaka ya vijiji 127 katika wilaya za Kilombero (65), Ulanga (40) na Malinyi (22) zimefanyika pamoja na kuandaa mipangokina ya makazi ya vijiji 99 katika Wilaya za Kilombero (54), Ulanga (31) na Malinyi (14).

Aidha, Mipango ya Matumizi ya Ardhi 245 imeandaliwa katika Wilaya za Misenyi (10), Bukoba (13) Muleba (21), Chato (17), Geita (2), Bukombe (6), Mbogwe (16), Nzega (11), Igunga (18), Iramba (18), Mkalama (6), Singida (20), Kondoa (7), Chemba (21), Hanang (8), Kiteto (16), Kilindi (7), Handeni (14), Korogwe (2) na Muheza (12).

Vilevile, hekta 350,576.05 zimetengwa kutoka katika vituo vya kupumzishia mifugo, Ranchi za Taifa, Mashamba ya TALIRI na Mashamba ya Kuzalisha Mifugo (LMUs) ili yatumiwe na wafugaji kwa utaratibu maalum na hekta 2,788,901.17 zimetengwa kwa ajili ya ufugaji katika Mikoa 22.

Aidha, katika kuwezesha Bodi za Maji za Mabonde kuunda Jumuiya za Watumia maji, majukwaa mapya katika Bodi za Maji za Mabonde ya Wami-Ruvu, Ziwa Victoria na Mto Rufiji pamoja na Vidaka Maji vya Mto Songwe, Mto Luiche na Mto Katuma katika Bonde la Ziwa Rukwa; Mto Kiwira na Mto Ruhuhu katika Bonde la Ziwa Nyasa yalianzishwa. Mapendekezo yanayotolewa katika majukwaa hayo, huchukuliwa na Wizara na yamekuwa na umuhimu mkubwa katika kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji.

Kuhusu suala la usimamizi wa vyanzo vya maji na ardhi katika mabonde, Bodi ya Maji ya Bonde la Wami/Ruvu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Mkina na Tanga Jiji imejenga mabirika matatu (3) ya kunyweshea mifugo katika Wilaya za Muheza, Mkinga na Tanga Jiji; kuhifadhi hekta 353 katika Wilaya ya Muheza na Morogoro; pamoja na kurejesha uoto wa asili katika vyanzo vya maji baada ya kutenga ardhi kwa ajili ya kilimo, malisho na mapito ya mifugo; na kuanzisha Klabu 36 za uhifadhi wa mazingira katika shule za msingi na sekondari.

ii. **Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji:**
Ujenzi wa miundombinu 16 ya skimu za umwagiliaji zenye thamani ya shilingi 6,500,000,000 katika Halmashauri 12 umefikia wastani wa asilimia 43.98. Aidha, Ukarabati wa malambo matatu katika Wilaya za Chato na

Butiama na ujenzi wa visima virefu viwili katika Wilaya ya Iringa na Manyoni unaendelea.

2.1.2 Mafanikio

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa **Eneo Kuu la Kwanza** la ASDP II ni pamoja na: -

i. Idadi ya wananchi wenye hati za kimila vijijini imeongezeka ambapo hati za Kimila zipatazo 308,549 zimetolewa. Hii imewezesha kuongezeka kwa usalama wa umiliki wa ardhi hasa maeneo ya vijijini, kupungua kwa migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya wakulima, wakulima na wafugaji na baina ya wafugaji ambapo kesi za migogoro ya matumizi ya ardhi zilipungua kutoka kesi 23,999 mwaka 2017/2018 hadi kesi 22,579 mwaka 2018/2019. Mipango hiyo imepunguza migogoro ya matumizi ya ardhi kwa asilimia sita (6); na
ii. Udhibiti wa upotevu wa maji na usimamizi wa miundombinu ya umwagiliaji umeimarika katika maeneo mbalimbali nchini.

2.1.3 Changamoto

Baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa eneo la Usimamizi wa Matumizi Endelevu ya Maji na Ardhi ni pamoja na:

i. Ongezeko la mahitaji ya ardhi kwa ajili ya matumizi ya ufugaji na kilimo ikilinganishwa na maeneo yaliyotengwa;
ii. Uvamizi wa maeneo ya hifadhi na vyanzo vya maji kwa shughuli za kilimo na ufugaji; na
iii. Kutokuwa na mipango ya matumizi ya ardhi kwenye baadhi ya maeneo.

2.2 Eneo Kuu la Pili: Kuongeza Tija na Faida Katika Kilimo, Mifugo na Uvuvi

Lengo la Eneo Kuu la Pili la ASDP II ni kuongeza uzalishaji na tija katika Sekta ya Kilimo ili kuongeza biashara na masoko kwa mazao ya kipaumbele. Vipaumbele vilivyozingatiwa ni vinne ambavyo ni kuendeleza na kuimarisha shughuli za utafiti; kuimarisha huduma za ugani na mafunzo na kuendeleza upatikanaji wa taarifa; kuwezesha upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora, pembejeo na huduma za afya; na kuimarisha usalama wa chakula na lishe.

Katika kutekeleza **Eneo Kuu la Pili** la ASDP II, jumla ya shilingi 74,926,179,280 ziliidhinishwa kwenye bajeti za Wizara za Sekta ya Kilimo kwa Mwaka wa fedha 2018/2019. Katika kipindi hicho, shilingi 34,002,069,121 zilitolewa sawa na asilimia 45.4 ya fedha zilizoidhinishwa na shilingi 33,728,627,837 zilitumika sawa na asilimia 99.2 ya fedha zilizotolewa. *(Jedwali Na. 3).*

Jedwali Na. 3: Vipaumbele na Bajeti katika Eneo Kuu la Pili

Vipaumbele na Bajeti katika Eneo Kuu la Pili laKuongeza Tija na Faida

Eneo la Kipaumbele	Fedha iliyoidhinishwa (TZS)	Fedha iliyotolewa (TZS)	Fedha iliyotumika (TZS)
Kuimarisha huduma za ugani na mafunzo na kuendeleza upatikanaji wa taarifa za kilimo, mifugo na uvuvi	23,406,734,000	12,609,782,237	12,609,782,237
Kuwezesha upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora na pembejeo za kilimo, mifugo, uvuvi na huduma za afya	3,895,160,000	2,313,308,086	2,313,308,086
Kuendeleza na kuimarisha shughuli za utafiti	1,803,844,774	-	-
Kuimarisha usalama wa chakula na lishe	45,820,440,506	19,078,978,798	18,805,537,514
Jumla ndogo	**74,926,179,280**	**34,002,069,121**	**33,728,627,837**

2.2.1 Kazi zilizotekelezwa

i. **Kuendeleza na kuimarisha shughuli za utafiti:**
Tafiti tano za uvuvi wa samaki aina ya pweza, jodari na jamii zake, samaki wanaopatikana kwenye matumbawe na kambamiti zimefanywa na TAFIRI katika maeneo ya Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi; Tafiti tatu za kuendeleza viwanda na ubunifu wa teknolojia rahisi za kupura, kupandia na kukausha mihogo, kukamua karanga na kubebea mazao kutoka shambani pamoja na tafiti za mahitaji ya zana za kilimo zimefanywa na Taasisi za CAMARTEC, TIRDO, TEMDO na SIDO.

Aina nne za mbegu bora za Mahindi za WE5135, WE5141, WE7118 na WE7133 zimegunduliwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI). TARI inaendelea na utaratibu wa kuzalisha kwa wingi mbegu hizo ili kuzifikisha kwa wakulima kwa wingi. Vilevile, TALIRI imefanya tafiti nane za kuboresha mbari (*genetics*) za ng'ombe wa maziwa na nyama, kuku, mbuzi na kondoo, uzalishaji wa punda, malisho bora na vyakula vya mifugo katika mikoa 16 kwa lengo la kuongeza tija na uzalishaji wa mifugo.

ii. **Kuimarisha huduma za ugani na mafunzo na kuendeleza upatikanaji wa taarifa za kilimo, mifugo na uvuvi:**

Kudahili wanafunzi 2,536 katika vyuo vya Mifugo (LITA) na wanafunzi 2,031 katika vyuo vya Kilimo (MATI) kwa ngazi ya Cheti na Stashahada na wanafunzi 1,500 katika Vyuo vya Mafunzo ya Uvuvi (FETA). Jumla ya Watumishi 24 wamepata ufadhili wa Serikali na kujiunga na masomo ya Shahada za Uzamili (18) na Shahada za Uzamivu (6) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (22), Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (1) na Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini Dodoma (1).

Huduma za ugani katika sekta ya uvuvi, mafunzo ya ulinzi wa rasilimali za uvuvi kwa vikundi 50 vya Ulinzi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (*Beach Management Unit - BMU*) zilitolewa katika Halmashauri za Wilaya za Pangani, Mkinga, Bagamoyo, Lindi Vijijini na Halmashauri ya Jiji la Tanga. Vilevile, elimu kuhusu ufugaji wa kisasa ilitolewa kwa wafugaji 20,239 na wagani 185 katika sekta ya mifugo katika Halmashauri zote nchini. Pia wagani 258 katika sekta ya kilimo eneo la mazao walipatiwa mafunzo ya muda mfupi katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Mtwara, Ruvuma, Tabora, Kigoma, Manyara, Simiyu na Geita. Kadhalika, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA) ilitoa mafunzo ya ukaguzi wa mbolea kwa maafisa kilimo 50 kutoka Mikoa 18 nchini.

iii. Kuwezesha upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora na pembejeo za kilimo, mifugo, uvuvi na huduma za afya:

Lita 140,000 za viuatilifu zilinunuliwa na kusambazwa katika Kanda ya Ziwa, Kanda ya Nyanda ya Juu Kusini, Kanda ya Kati, Kanda ya Magharibi, Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Mashariki kwa ajili ya kudhibiti Viwavijeshi Vamizi; na tani 492,394 za aina mbalimbali za mbolea zilinunuliwa na kusambazwa katika mikoa yote nchini.

Ili kudhibiti magonjwa yatokanayo na kupe, lita 8,823.53 za madawa ya kuua kupe zilinunuliwa na kusambazwa katika majosho 1,486 yanayofanya kazi katika mikoa 24; majosho 151 yalikarabatiwa; kamati 847 za ufuatiliaji wa majosho pamoja na akaunti vilianzishwa na ujenzi wa maabara iliyopo Kibaha ya kutengeneza chanjo za mifugo umefikia asilimia 24. Jumla ya dozi 39,548,000 ya chanjo ya magonjwa ya mifugo zilizalishwa na kusambazwa kwa wafugaji. Pia jumla ya tani 12.1 za mbegu bora za malisho zilizalishwa kutoka katika mashamba ya Serikali na kusambazwa kwa wafugaji.

Vifaranga vya samaki milioni 17.4 vilizalishwa na kusambazwa kwa wafugaji wa samaki. Uzalishaji wa samaki wa kufugwa uliongezeka kutoka tani 14,800 hadi tani 18,081.6; tani 336.4 za kambamti wa kufugwa zimevunwa katika shamba la Jimbo lililopo Wilayani Mafia-Pwani; na idadi ya mabwawa ya kufuga samaki iliongezeka kutoka 24,302 hadi 26,445.

2.2.2 Mafanikio

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji eneo la kuongeza tija na faida kwenye mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi ni pamoja na: -

- Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula nchini hadi kufikia tani milioni 16.9 ikilinganishwa na mahitaji ya chakula nchini ambayo ni tani milioni 13.6, sawa na ziada ya tani milioni 3.3. Kiwango cha utoshelevu wa chakula kwa msimu wa mwaka 2018/2019 kilikuwa asilimia 124. Kiwango hiki kimeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2017/2018 ambapo kiwango kilikuwa ni asilimia 123;
- Kuimarika kwa hifadhi ya chakula ya Taifa ambapo NFRA ilinunua tani 46,321 za mahindi;
- Udhibiti wa magonjwa ya mifugo yanayosababishwa na kupe ambapo michovyo milioni 40.4 ilifanyika hivyo kuongeza thamani ya mifugo katika soko na kuongezeka kwa koo za mitamba kutoka 13,735 hadi 15,097 na;
- Kupungua kwa uvuvi haramu kwa asilimia 75 katika maji baridi na kupungua kwa milipuko katika uvuvi kwa asilimia 99 katika mwambao wa bahari kutokana na operesheni Sangara 1 na 2.

2. 2.3 Changamoto

Changamoto zilizojitokeza katika eneo la Kuongeza Tija na Faida Katika Kilimo, Mifugo na Uvuvi ni pamoja na:

i. Usambazaji usiotosheleza na matumizi yasioridhisha ya teknolojia bora za kilimo, mifugo na uvuvi;
ii. Matokeo ya utafiti kutowafikia walengwa kwa wakati;
iii. Upungufu mkubwa wa maafisa ugani; na
iv. Uwekezaji na uwezo mdogo katika kununua pembejeo, madawa ya kilimo na mifugo na uvuvi wa bahari kuu.

2.3. Eneo Kuu la Tatu: Upatikanaji wa Masoko na Uongezaji wa Thamani

Lengo la Eneo la Tatu la ASDP II ni kuongeza thamani ya mazao kwa kuhamasisha ushindani wa sekta binafsi na vyama vya wakulima, wafugaji na wavuvi vyenye ufanisi. Vipaumbele vilivyozingatiwa katika eneo hili ni kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi na kuendeleza usindikaji na kuongeza thamani kwa bidhaa zitokanazo na mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Katika kutekeleza Eneo Kuu la Tatu la programu, jumla ya Shilingi 251,458,767,531 ziliidhinishwa kwenye bajeti za Wizara za Sekta ya Kilimo. Kati ya hizo, shilingi 193,624,028,665 zilitolewa sawa na asilimia 77 ya fedha zilizoidhinishwa. Jumla ya shilingi 193,624,028,665 zilitumika, sawa na asilimia 100 ya fedha zilizotolewa. *(Jedwali Na. 4)*.

Jedwali Na. 4: Vipaumbele na Bajeti katika Eneo Kuu la Tatu

	Vipaumbele na Bajeti katika Eneo Kuu la Tatu la Kuongeza Upatikanaji wa Masoko na Uongezaji wa Thamani			
	Eneo la Kipaumbele	**Fedha iliyoidhinishwa (TZS)**	**Fedha iliyotolewa (TZS)**	**Fedha iliyotumika (TZS)**
1	Kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi	217,842,955,000	173,139,680,000	173,139,680,000
2	Kuendeleza usindikaji na kuongeza bidhaa zitokanazo na mazao, mifugo na uvuvi	33,615,812,531	20,484,348,665	20,484,348,665
	Jumla ndogo	**251,458,767,531**	**193,624,028,665**	**193,624,028,665**

2.3.1 Kazi zilizotekelezwa

i. Kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi:

Ujenzi na ukarabati wa minada ya mifugo mitano katika maeneo ya Kirumi, Longido, Nyamatala, Buhigwe na Kasesya umefikia katika hatua mbalimbali za ujenzi; masoko ya mazao 7 yamejengwa na kukamilika wilayani Karatu (1), Lushoto DC (1), Makambako TC (1), Tabora MC (1), Tunduma TC (1), Mpanda DC (1) na Bukombe DC (1) na masoko 8 yanaendelea kujengwa wilayani Kibaha (1), Kigoma DC (2), Momba DC (1), Buhigwe DC (1), Chalinze (1), Kongwa (1) na Morogoro MC (1). Maghala 6 yamejengwa wilayani Sumbawanga DC (1), Kilosa DC (1), Mpanda DC (3) na Kakonko DC (1) na Maghala saba yamekarabatiwa wilayani Mpimbwe DC. Barabara yenye urefu wa kilomita 15 katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe DC imekamilika ambayo imeunganisha masoko ya Uyovu, Kayenze na Kabogole.

Mfumo wa Stakabadhi ghalani umetumika katika kuuza zao la korosho na ufuta katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Manyara na Dodoma ambapo jumla ya AMCOS 5 zilipata mafunzo ya kuweka madaraja ya zao la korosho. Aidha, wakulima 10,002 wa zao la muhogo kati ya wakulima 10,126 waliunganishwa na watoa huduma za pembejeo katika maeneo yanayozalisha korosho na ufuta. Vilevile, Shirika la Viwango nchini (TBS) iliandaa viwango 75 kati ya hivyo viwango 20 vilikuwa vya Sekta ya Nguo na Ngozi na viwango 55 vya Sekta ya Kilimo na Chakula. Pia, jumla ya leseni za nembo ya ubora wa TBS 143 zilitolewa kati ya hizo leseni 15 zimetolewa kwa

wajasiriamali wadogo kwenye Sekta ya Kilimo. Hali kadhalika, wakulima na wafanyabiashara wa viungo 50 walipata oda ya kuuza tani 200 za viungo kwa kupitia mkataba kati ya Kampuni ya *Sustainable Agriculture of Tanzania* na Kampuni ya Zanzibar.

Katika kuboresha ufikiwaji wa masoko na usafirishaji wa bidhaa za kilimo vijijini, matengenezo ya jumla ya Kilometa 22,917.67 za barabara za vijijini na mijini ambayo yanajumuisha matengenezo ya mara kwa mara, matengenezo ya maeneo korofi na matengenezo ya muda/misimu yalifanyika. Vilevile, matengenezo na ukarabati wa vivuko na madaraja mbalimbali yalifanyika (*1877 Lines,120 Bridges repair,117 New Bridges,395 BC,67,844m Drain,5 Bridges designs,7 stone pitching projects 3358sqm drainage structures and 202 bicons).*

ii. Kuendeleza usindikaji na kuongeza bidhaa zitokanazo na mazao, mifugo na uvuvi:

Kupatikana kwa ekari 107 eneo la Zuzu katika Mkoa wa Dodoma kwa ajili ya usindikaji wa ngozi na bidhaa za ngozi na ujenzi wa viwanda vinne vya kubangua korosho katika Mkoa wa Lindi na Mtwara kupitia SIDO.

iii. Miundombinu ya Masoko, kuongeza thamani na uwezeshaji wa fedha vijijini:

Kupitia program ya *Marketing Infrastructure, Value Addition and Rural Finance – MIVARAF,* vikundi vitano viliwezeshwa kununua mitambo ya kuchakata mazao ambapo mitambo minne ilinunuliwa na kusimikwa. Vilevile, mafunzo kwa washiriki 678 kuhusu uongezaji thamani yalifanyika na jumla ya vikundi 2,331 vyenye zaidi ya walengwa 86,000 vilijengewa uwezo jinsi ya kupanga na kulifikia soko na kuongeza thamani ya bidhaa zao.

2.3.2 Mafanikio

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa **Eneo Kuu la Tatu** la ASDP II ni pamoja na: -

- Usindikaji wa maziwa uliongezeka kutoka lita milioni 56 katika mwaka 2017/18 hadi lita milioni 66.9 katika mwaka 2018/19, sawa na asilimia 19.4;
- Uzalishaji wa zao la nyama umeongezeka kutoka tani 679,992 katika mwaka 2017/18 hadi kufikia tani 690,629 katika mwaka wa fedha 2018/19, sawa na asilimia 1.54;
- Mfumo wa Stakabadhi Ghalani na kuanzishwa kwa Soko la Bidhaa umewezesha kuimarika kwa bei ya ufuta kutoka wastani wa shilingi 1,500 hadi shilingi 3,195 kwa kilo na;
- Kupatikana kwa ajira ya watu 411 katika viwanda vya kubangua korosho katika Mikoa ya Mtwara na Lindi.

2.3.3 Changamoto

- Uelewa mdogo wa wananchi katika matumizi ya maghala; ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika ujenzi wa miundombinu ya masoko;
- Uzalishaji wa mazao usiokidhi viwango na ubora unaohitajika katika soko; uzalishaji usiokidhi mahitaji ya soko; na
- Viwanda kuendeshwa chini ya uwezo kutokana na uhaba wa malighafi.

2.4 Eneo Kuu la Nne Kuiwezesha Sekta katika Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini

Lengo la Eneo la Nne la ASDP II ni kuboresha mazingira ya uwekezaji katika kilimo, mifugo na uvuvi. Vipaumbele vilivyozingatiwa katika eneo hili ni pamoja na: Kuboresha Sera, Mfumo wa Usimamizi na Mazingira ya Biashara; kuimarisha miundo na uwezo wa kitaalam kwa vikundi na Vyama vya Ushirika vilivyopo na vipya vya wazalishaji, wafanyabiashara na wasindikaji wadogo; Kuboresha uwezo na usimamizi wa mifumo ya ukusanyaji na utunzaji wa takwimu za Sekta ya Kilimo; na Kuweka mifumo imara ya ufuatiliaji na tathmini katika kilimo, mifugo la uvuvi.

Katika kutekeleza Eneo Kuu la nne la ASDP II, jumla ya Shilingi 62,576,866,486 ziliidhinishwa kwenye bajeti za Wizara za Sekta ya Kilimo. Kati ya hizo shilingi 2,444,531,173 zilitolewa sawa na asilimia 3.9. Aidha, shilingi 2,414,531,173 zilitumika sawa na asilimia 98.7 ya fedha zilizotolewa. (Jedwali Na. 5).

Jedwali Na. 5: Vipaumbele na Bajeti katika Eneo Kuu la Nne

Vipaumbele na Bajeti katika Eneo Kuu 4: Kuiwezesha Sekta Katika Uratibu, Ufuatiliaji na Tathimini				
Na.	**Eneo la Kipaumbele**	**Fedha iliyoidhinishwa (TZS)**	**Fedha iliyotolewa (TZS)**	**Fedha iliyotumika (TZS)**
1	Kuboresha Sera na Mfumo wa Usimamizi na Mazingira ya Biashara	2,144,320,000	1,500,000,000	1,500,000,000
2	Kuboresha na kuimarisha uratibu (kutoka Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa) na uratibu kati ya ASLMs	57,858,645,766	202,000,000	202,000,000

Vipaumbele na Bajeti katika Eneo Kuu 4: Kuiwezesha Sekta Katika Uratibu, Ufuatiliaji na Tathimini				
Na.	**Eneo la Kipaumbele**	**Fedha iliyoidhinishwa (TZS)**	**Fedha iliyotolewa (TZS)**	**Fedha iliyotumika (TZS)**
3	Kuboresha uwezo na usimamizi wa mifumo ya ukusanyaji na utunzaji wa takwimu za sekta ya kilimo	1,705,351,173	380,531,173.00	380,531,173.00
4	Kuimarisha uwezo wa taasisi na wa kiufundi wa wazalishaji	310,000,000	310,000,000	280,000,000
5	Kuweka mifumo imara ya ufuatiliaji na tathmini katika Sekta ya Kilimo	185,980,720	-	-
7	Uboreshaji wa TEHAMA kwa huduma na mifumo ya taarifa za kilimo	355,068,827	52,000,000	52,000,000
8	Kukuza na kuimarisha ushirikiano wa kijinsia katika sera ya kilimo	17,500,000	-	-
Jumla ndogo		**62,576,866,486**	**2,444,531,173**	**2,414,531,173**

2.4.1 Kazi zilizotekelezwa

i. Sera na Sheria zifuatazo zimepitiwa kwa lengo la kuboreshwa;

a) Sera ya Uvuvi ya Mwaka 2015 imefanyiwa tafsiri kwa lugha ya Kiswahili; Sera ya Kilimo 2013 inafanyiwa mapitio; Sera ya mifugo ya mwaka 2006 inafanyiwa mapitio; Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya mwaka 1996 inafanyiwa mapitio; Sera ya Biashara ya mwaka 2003 inafanyiwa mapitio; Sera ya Viwanda vidogo na biashara ndogo ya mwaka 2003 inafanyiwa mapitio; Sheria ya Hifadhi ya Maeneo Tengefu Na. 29 ya mwaka 1994 inafanyiwa mapitio; Sheria ya Ngozi Na.18 ya mwaka 2008 inafanyiwa mapitio, Sheria ya Mbari za Wanyama ya mwaka 2018 inaandaliwa; na Kanuni sita za maziwa zimepitiwa upya. Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma ya mwaka 1998 inafanyiwa mapitio na Sera ya Ardhi ya mwaka 1995 inapitiwa.

b) Kuondoa tozo 114 kutoka katika Sekta ya Kilimo na Mifugo.

c) Kuanzishwa kwa vituo vya mipakani vya Mtukula, Namanga, Mtambaswala, Rusumo na Tunduma;

d) Kupunguza vizuizi vya barabarani kutoka 15 hadi vitatu; na

e) Kudhibiti biashara haramu ya mifugo kwenye mikoa 18 kwa kufanya operesheni maalum (Nzagamba II) na hivyo kuokoa mapato ya Serikali yanayofikia shilingi Bilioni 38.5.
f) Kuandaa mwongozo wa uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ya Wilaya (DADPs).

ii. Kuboresha uwezo na usimamizi wa mifumo ya ukusanyaji na utunzaji wa takwimu za sekta ya kilimo:

Mifumo ya Ukusanyaji, Uhifadhi, Uchambuzi na Usambazaji wa Taarifa na takwimu za Kilimo (*Agricultural Routine Data System - ARDS, Livestock Information Network and Knowledge System – LINKS, Marketing Information System – MIS)* imeimarishwa kwa kuwezesha upatikanaji wa takwimu kutoka kwenye Halmashauri. Aidha, Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Ukuzaji Viumbe Maji umefanyiwa mapitio kwa lengo la kuuboresha.

iii. Kuimarisha Miundo na Uwezo wa Kitaalam kwa Vikundi na Vyama vya Ushirika vilivyopo na vipya vya wazalishaji, wafanyabiashara na wasindikaji wadogo

Vyama vya ushirika vimeongezeka kutoka 10,990 mwaka 2017 hadi 11,331 mwaka 2018; Idadi ya wanachama wa vyama vya ushirika imeongezeka kutoka 2,619,311 mwaka 2017 hadi kufikia 3,998,193 mwaka 2019; na vikundi vya wakulima vya ushirika 20, vyama vya wazalishaji, wafanyabiashara na Wasindikaji wadogo vimeimarishwa ikiwa ni pamoja na kupewa mafunzo kuhusu wajibu na majukumu yao, utawala bora na uongozi.

2.4.2 Mafanikio

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa **Eneo Kuu la Nne** la ASDP II ni pamoja na: -

- Kuongezeka kwa uwazi katika ufanyaji biashara za mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi;
- Kuongezeka kwa maduhuli ya Serikali;
- Kuimarika kwa Mfumo wa Usimamizi na Udhibiti katika Sekta ya Kilimo;
- Kurahisisha biashara mipakani na ndani ya nchi na;
- Kuimarika kwa upatikanaji na usambazaji wa taarifa za kisekta.

2.4.3 Changamoto

- Kushindwa kupata mrejesho wa taarifa za sekta kwa wakati;
- Kutopatikana kwa takwimu na taarifa sahihi za sekta kwa wakati;
- Kutopatikana kwa mikopo (masharti na utayari wa kukopa) kwa wadau wa Sekta ya Kilimo.

SEHEMU YA TATU

3.0 USHIRIKI WA SEKTA BINAFSI NA WASHIRIKA WA MAENDELEO

Sekta binafsi ina umuhimu mkubwa katika utekelezaji wa Programu ya ASDP II ikijihusisha katika shughuli mbalimbali za kiuchumi katika sekta ya kilimo ikiwemo uzalishaji, usindikaji, uhifadhi na uuzaji wa mazao na bidhaa za kilimo, mifugo na uvuvi; uwezeshaji katika kutoa na kutumia huduma mbalimbali zikiwemo huduma za kifedha na kiufundi kwa wadau wa sekta ya kilimo.

Kumekuwa na changamoto ya uratibu wa shughuli za sekta binafsi katika sekta ya kilimo ikiwemo upatikanaji wa taarifa na takwimu sahihi. Juhudi mbalimbali ikiwemo kuanzishwa kwa madawati ya Sekta Binafsi kwa Wizara za Kisekta. Hivyo, katika taarifa hii, takwimu za sekta binafsi zinazowasilishwa ni zile zilizopatikana kutoka Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambapo zinaonesha katika mwaka wa fedha wa 2018/2019, Sekta Binafsi iliwekeza jumla ya Shilingi 53,249,400,000.

Jedwali Na. 6: Uwekezaji wa Sekta Binafsi

Uwekezaji wa Sekta Binafsi			
Eneo la Kipaumbele la ASDP II	**Taasisi ya Sekta Binafsi**	**Utekelezaji**	**iliyotumika Shilingi (000)**
Kuongeza tija na faida katika kilimo, mifugo na uvuvi	Galaxy	Ujenzi wa Kiwanda cha Maziwa Jijini Arusha	5,500,000.00
	Tanga Fresh	Ununuzi wa mitamba ya ng'ombe wa maziwa 73 kutoka Rungwe Mbeya	131,400.00
Kuboresha biashara, kuongeza thamani ya mazao na masoko	ASAS	Kufunga Mitambo ya *Ultra Heat Treatmen* t (UHT) yenye uwezo wa	13,000.00
	Elia Food and Overseas Ltd	Ujenzi wa kiwanda cha kuchakata nyama - Longido	11,500,000.00
	TAN CHOICE (Kibaha-Pwani)	Ujenzi wa kiwanda cha kuchakata nyama - Kibaha	12,650,000.00
	Taasisi za Fedha	Kutoa Mikopo kwa wadau mbalimbali wa Sekta za Kilimo.	22,000,000.00
Utoaji wa Hati za Haki Miliki za Kimila	Kampuni ya *Land Tenure Assistance*	Kupima maeneo ya ardhi ili kutoa Hati za Hakimiliki za Kimila.	1,455,000.00
Jumla			**53,249,400.00**

3.1 Mafanikio

- Kusaidia kuongeza uzalishaji na uchakataji wa nyama na maziwa
- Kuongeza wigo wa upatikanaji fedha kwa wadau wa Sekta ya Kilimo
- Kusaidia harakati za kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi

3.2 Changamoto

- Kutopatikana kwa taarifa za Sekta binafsi kutoka Wizara za Sekta ya Kilimo
- Uhamishaji mdogo Sekta Binafsi kujua nafasi yake kwenye utekelezaji wa programu
- Miamvuli ya Sekta Binafsi kutokuwa na takwimu za uwekezaji kwenye Sekta ya Kilimo

4.0 USHIRIKI WA WASHIRIKA WA MAENDELEO

Mchango wa washirika wa maendeleo kwa mwaka 2018/2019 kwa maeneo makuu ya ASDP II umeoneshwa kwenye *Jedwali Na. 1*. Katika jedwali inaonekana kuwa kiasi cha shilingi 66,494,641,531 ziliidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza miradi na shughuli mbalimbali za programu ambapo kiasi cha shilingi 31,517,341,463 zimetolewa sawa na asilimia 47. Aidha, kiasi cha shilingi 29,290,506,674 zimetumika sawa na asilimia 93 ya fedha zilizotolewa.

4.1 Mafanikio

- Washirika wa Maendeleo kuendelea kuchangia bajeti ya Programu

4.2. Changamoto

- Kutopatikana kwa taarifa za utekezaji wa Programu kwa miradi inayotekelezwa nje ya mfumo wa bajeti.
- Kutofikiwa lengo la utoaji fedha kulingana na mpango kazi na bajeti ya ASDPII

5.0 CHANGAMOTO ZA JUMLA ZILIZOKABILI UTEKELEZAJI WA ASDPII

Pamoja na changamoto zinazokabili utekelezaji wa ASDPII ambazo zimeoneshwa katika kila eneo, zipo changamoto nyingine za jumla ambazo zinaikabili Programu hii. *Jedwali Na. 7* linaonesha changamoto za ujumla zilizojitokeza kwenye utekelezaji wa ASDP II kwa mwaka 2018/19 na hatua za kuzitatua changamoto hizo.

Jedwali Na. 7: Changamoto za jumla katika utekelezaji wa ASDP II kwa mwaka 2018/2019

Na.	Changamoto	Mapendekezo ya hatua za kutatua changamoto
1	Upatikanaji mdogo wa fedha kwa kuzingatia mahitaji ya programu.	• Kuandaa Mwongozo wa Kutafuta Rasilimali fedha • Kuhamasisha Benki za Biashara na Mifuko ya Kijamii kuwekeza kwenye kilimo, mifugo na uvuvi kwa kutoa mikopo nafuu kwa wawekezaji kwenye Sekta Binafsi. • Majadiliano na Makubaliano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo kuongeza mchango

Na.	Changamoto	Mapendekezo ya hatua za kutatua changamoto
		kwenye bajeti ya ASDPII • Serikali kutoa fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa programu
2	Uwekezaji Mdogo wa Sekta binafsi katika Kilimo	• Kuboresha mazingira ya Kisera ikiwa ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa *Blueprint*; • Kuwepo kwa majukwaa ya kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi; • Serikali kuweka dhamana ili kuwezesha taasisi za fedha kuongeza mitaji na kupunguza riba katika mikopo ya kilimo.
3	Upatikanaji hafifu wa takwimu za uwekezaji wa sekta binafsi katika sekta ya kilimo.	• Wizara za Sekta ya Kilimo ziimarishe upatikanaji wa taarifa za sekta binafsi kwa kuanzisha madawati ya Sekta Binafsi au kupitia bodi za mazao. • Kuimarisha mifumo ya ukusanyaji, uhifadhi, uchambuzi na usambazaji wa takwimu na taarifa za kilimo, mifugo na uvuvi katika Wizara za Sekta ya Kilimo • Kufanyika kwa zoezi la kuwatambua wadau wote hasa Taasisi na Asasi zisizo za Serikali zinazoendesha miradi ya kilimo yenye mwelekeo wa kutekeleza ASDPII katika maeneo mbalimbali nchini
4	Muunganiko hafifu wa wadau kwenye utekelezaji wa Programu.	• Kuimarisha uratibu wa programu kitaifa na kwenye ngazi ya Halmashauri kwa kuhakikisha ushirikishwaji wa wadau kupitia mikutano rasmi ya programu. • Kuandaa mkakati wa mawasiliano wa programu

6.0 HITIMISHO

Katika mwaka 2018/2019, utekelezaji wa Programu ya ASDP II umekuwa na mafanikio chanya kwenye maeneo ulikotekelezwa. Hata hivyo, uidhinishwaji na utoaji mdogo wa fedha unaonesha ugumu wa utekelezaji ikilinganishwa na mahitaji ya programu kwa ujumla wake. Pamoja na changamoto mbalimbali zilizojitokeza na ambazo zimeelekezewa namna ya kuzitatua, ipo haja ya kujenga uelewa kwa wadau kuhusu namna ya utekelezaji wa Programu unavyopaswa kwa kuzingatia dhana ya Mfuko wa Pamoja (Basket Fund), Washirika wa Maendeleo kuweza kutekeleza miradi ya ASDPII nje ya mfumo wa bajeti na nafasi kubwa iliyonayo Sekta Binafsi katika utekelezaji wa programu.